**BARAZA LA TAIFA LA HUDUMA JUMUISHI ZA FEDHA**

# TUZO ZA HUDUMA JUMUISHI ZA FEDHA TANZANIA (TFIA) ZA MWAKA 2025

## Utangulizi

Baraza la Taifa la Huduma Jumuishi za Fedha linapenda kutangaza mwito rasmi wa kupokea maombi kwa ajili ya Tuzo za Huduma Jumuishi za Fedha Tanzania (TFIA) za Mwaka 2025. Tuzo hizi zinatambua juhudi za watu binafsi na taasisi katika kuendeleza huduma jumuishi za fedha nchini Tanzania, kwa kuhamasisha upatikanaji na utumiaji wa huduma rasmi za fedha kwa makundi yasiyohudumiwa au yanayohudumiwa kwa kiwango kidogo. Baraza litatoa tuzo zinazohusu huduma na bidhaa za kifedha kutoka sekta ndogo ya fedha ya benki, huduma ndogo za fedha, masoko ya mitaji, bima, na hifadhi ya jamii.

Dirisha la maombi limefunguliwa rasmi kuanzia tarehe **04 Julai hadi 31 Julai 2025**. Watu na taasisi zote zinazostahili zinakaribishwa kuwasilisha maombi yao kupitia kiunganishi kifuatacho:

**Bonyeza hapa kuwasilisha maombi**

## Lengo la Tuzo

Lengo la Tuzo za Huduma Jumuishi za Fedha ni kutambua watu binafsi na taasisi ambazo zimeonyesha jitihada katika kuendeleza na kutekeleza mbinu bora zinazokabiliana na changamoto za huduma jumuishi za fedha kupitia kuandaa, kutekeleza, na kuhamasisha programu, bidhaa, huduma, sera na kanuni zenye mchango mkubwa katika kukuza huduma jumuishi za fedha nchini.

## Misingi Mwongozo

Misingi inayoongoza utoaji wa tuzo hizi ni: **lengo, usawa, ujumuishaji, athari chanya, ubora, na ushirikiano**. Vigezo hivi vinahakikisha kuwa tuzo zinatolewa kwa haki na kwa makundi yasiyopata huduma za fedha kwa usawa kama wengine.

**Wigo wa Tuzo**

Tuzo hizi zinawalenga watu binafsi na taasisi kutoka sekta ya benki, huduma ndogo za fedha, hifadhi ya jamii, bima, na masoko ya mitaji, pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) na washiriki kutoka Taasisi zisizo za sekta ya fedha kama vile viwanda, utalii, usafirishaji, biashara za jumla na rejareja, kilimo, mawasiliano na teknolojia ya habari, michezo na burudani, ambazo huchangia kwa kiasi kikubwa katika kukuza huduma jumuishi za fedha nchini.

Kwa upekee, tuzo hizi zitaangazia: makundi yaliyoachwa nyuma zaidi katika kufikiwa na kutumia huduma rasmi za fedha, ubunifu wa kiteknolojia ya masuala ya fedha, elimu ya fedha na utatuzi wa malalamiko, tafiti zinazohusiana na huduma za fedha, uhamasishaji wa masuala ya huduma za fedha, pamoja na uvumbuzi wa sera na kanuni zinachochea huduma rasmi za fedha.

**Vipengele vya Tuzo**

1. Tuzo ya kuongeza Huduma Jumuishi za Fedha kwa Wanawake
2. Tuzo ya kuongeza Huduma Jumuishi za Fedha kwa Vijana
3. Tuzo ya kuongeza Huduma Jumuishi za Fedha kwa Watu Wenye Ulemavu
4. Tuzo ya Huduma Jumuishi za Fedha katika kuwawezesha Wafanyabiashara Wadogowadogo, Wadogo na Wakati kifedha
5. Tuzo ya kuongeza Huduma Jumuishi za Fedha Vijijini
6. Tuzo ya Huduma Jumuishi za Fedha kuhusu Teknolojia Shirikishi ya Fedha
7. Tuzo ya Huduma Jumuishi za Fedha kuhusu Uwezeshaji Endelevu
8. Tuzo ya Utatuzi wa Malalamiko ya Wateja wa Huduma za Kifedha
9. Tuzo ya Huduma Jumuishi za Fedha kuhusu utoaji wa Elimu ya Fedha
10. Tuzo ya Kutambua Mchango Maalum katika kuendeleza Huduma Jumuishi za Fedha nchini.

**Mchakato wa Tathmini**

Kila ombi litatathminiwa kwa kina na Kamati ya Tuzo pamoja na Jopo la Majaji, kwa kuzingatia wigo, athari yake kwa jamii na sekta ya fedha, na kiwango cha ubunifu . Lengo letu ni kutambua wale wanaoonyesha kujitolea kwa hali ya juu na mafanikio yanayoweza kupimika katika kuendeleza huduma jumuishi za fedha nchini.

**Rejea ya Tathmini**

Muda wa rejea kwa ajili ya tathmini kwa Tuzo za Huduma Jumuishi za Fedha kwa mwaka 2025 ni taarifa za kuanzia tarehe **01 Julai 2024 hadi 30 Juni 2025**, ili kupima maendeleo yaliyofikiwa katika kipindi cha mwaka mzima.

**Vigezo vya Kushiriki**

Ili kushiriki kikamilifu katika Tuzo hizi, tunakushauri kupitia **vigezo vya Tuzo** vinavyobainisha masharti na viwango vya kutambuliwa. Tembelea kiunganishi hiki kupata vigezo hivyo kwa kina:

https://www.bot.go.tz/Adverts/PressRelease/en/2024120315251343.pdf

**Mawasialiano**

Kwa maelezo zaidi au maswali kuhusu TFIA, tafadhali wasiliana nasi kwa:
**Simu:** +255-22-2235247

**Barua Pepe:** Fin.InclusionSecretariat@bot.go.tz